HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

Mhe. Mwenyekiti,
Wahe. Wajumbe
Baraza la Madiwani,
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela,
ILEMELA.

YAH: TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA NNE (APRILI – JUNI) YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 ILIYOWASILISHWA TAREHE 27/07/2017

1.0. UTANGULIZI

Mhe: Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa taarifa ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya Mwaka.

Hivyo taarifa hii itakuwa na mambo yafuatayo:-

i. *Taarifa ya uhakiki wa watumishi awamu ya II;*
ii. *Taarifa ya urasimishaji wa Makazi holela;*
iii. *Taarifa ya utatuzi wa Migogoro ya Ardhi;*
iv. *Taarifa ya ujio wa Mwenge wa Uhuru tarehe 21/08/2017;*
v. *Taarifa ya ujio wa wageni kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro tarehe 19/06/2017;*
vi. *Taarifa ya ujio wa ugeni toka nchi ya Korea Kusini tarehe 31/07/2017 hadi 04/08/2017; na*
vii. *Taarifa ya ujio wa ugeni toka nchini Uingereza shule rafiki ya Ibeshi shule ya Msingi (Derby Grammer School)*
viii. *Taarifa ya Mikutano ya Mhe: Mbunge wa Jimbo la Ilemela.*

2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

2.1.1 Taarifa ya uhakiki wa Watumishi awamu ya II

Mhe: Mwenyekiti, Katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni 2017, Halmashauri imeendelea kufanya uhakiki wa watumishi kwa watumishi wenye kiwango cha elimu ya Darasa la Saba walioajiriwa baada ya tarehe 20/05/2004 kwa kuzingatia maagizo ya viongozi wa Serikali, jumla ya watumishi 12 walioajiriwa baada ya tarehe tajwa hapo juu ambao hawakujiendeleza wamesimamishiwa mishahara na watumishi 7 ambao hawakuwasilisha vyeti wakati wa uhakiki pia wamesimamishiwa mishahara. Ufumbuzi wa suala hili tunasubiri maelekezo kutoka mamlaka za juu.

2.1.2 Taarifa ya urasimishaji wa Makazi holela katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri.

Mhe: Mwenyekiti, ili kudhibiti makazi yasiyo rasmi Halmashauri inaendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuboresha Makazi kwa kufanya upimaji shirikishi ambapo katika zoezi la kurasimisha makazi, viwanja 16,141 vilitarajiwa kupimwa na kupatiwa Hati ifikapo mwezi Juni 2017. Hadi sasa jumla ya viwanja 10,320 vimekwisha kupimwa na Hati 1,407 zimeandaliwa. Aidha, viwanja 18,495 viko kwenye hatua mbalimbali za upimaji na kufanya jumla ya viwanja 28,815 sawa na asilimia 179 ya lengo. Hii ina maana kuwa kama wananchi watakamilisha malipo ya michango yao kupimiwa na Hati, Halmashauri itavuka lengo la upimaji na utoaji wa Hati kwa asilimia 79.

2.1.3 Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

Mhe: Mwenyekiti, katika kushughulikia migogoro ya Ardhi, Halmashauri imeweka utaratibu wa kutembelea kata zote 19 ili kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi ya kata. Aidha, kuanzia mwezi Januari 2017 hadi Juni 2017. Jumla ya malalamiko ya wananchi 195, malalamiko ya

wananchi 183 yalipokelewa na kutolewa majibu kwa njia ya barua na malalamiko 12 yanaendelea kushughulikiwa.

- Malalamiko 67 yaliyopokelewa yalihusu uelewa mdogo wa Sheria za Ardhi juu ya utwaaji wa ardhi, ambapo wananchi maeneo yao yalitwaliwa na kugawiwa wakati wa Sheria ya Ardhi Namba. 113 ya Mwaka 1923;
- Malalamiko 52 yalihusu ugawaji wa ardhi uliofanyika kuanzia Mei 2001 ambapo Walalamikaji walielimishwa jinsi Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999 ilivyotambua thamani ya ardhi na maendelezo yote yaliyopo juu ya ardhi husika;
- Malalamiko 27 yalikuwa na mashauri katika Mahakama ambayo yalikuwa katika hatua tofauti tofauti za usikilizwaji, na
- Malalamiko 16 yalihusu migogoro ya mipaka ya ardhi baina ya majirani ambayo mingine ilitatuliwa kwa kupeleka Wapima wa Ardhi na mingine kupitia uongozi wa Mitaa na Kata.

2.1.4 Taarifa ya ujio wa Mwenge wa Uhuru tarehe 21/08/2017

Mhe: Mwenyekiti, kama ilivyo kawaida ya kila Mwaka ambapo Mwenge wa Uhuru hukimbizwa kila Wilaya nchini, Halmashauri yetu inatarajiwa kuupokea Mwenge wa Uhuru tarehe 21/08/2017 kutokea Wilaya ya Nyamagana. Mapokezi yatafanyika katika uwanja wa Nyakato karibu na Ofisi ya Mtendaji wa Kata na Mwenge wa Uhuru utakabidhiwa Wilaya ya Ukerewe hapo tarehe 22/08/2017.

Hivyo, natoa rai kwa viongozi wote wa vyama vya Siasa, Madhehebu ya Dini, Serikali kuanzia ngazi ya Mtaa, Kata na Wilaya pamoja na wananchi wote kushiriki kikamilifu katika Mbio za Mwenge wa Uhuru Mwaka 2017.

2.1.5 Taarifa ya ujio wa wageni kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro

Mhe: Mwenyekiti, Halmashauri yetu ilipokea wageni ambao ni Baraza la Madiwani kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro mnamo tarehe 19/06/2017. Lengo la ziara hiyo, lilikuwa ni kujifunza mambo mbalimbali yanayofanyika katika Halmashauri yetu ikiwa ni pamoja na kuona fursa za uwekezaji, ukusanyaji wa mapato, urasimishaji wa Makazi na mbinu zinazotumiwa na Halmashauri katika kukusanya na kuondosha taka ngumu.

Mhe: Mwenyekiti, Mapokezi yalifanyika vizuri ikiwa ni pamoja na uwasilishaji wa mada mbalimbali zilizohusu uwekezaji, ukusanyaji wa mapato, urasimishaji wa Makazi holela na suala la usafi wa mazingira. Kwa ujumla wageni walitoa shukrani zao za dhati kwa wataalam wa Halmashauri ya Manispaa kwa kuwapatia mafunzo na uelewa. Shukrani pia walizitoa kwa Mstahiki Meya, Naibu Meya na Baraza lote la Madiwani kwa kukubali kuwapokea.

2.1.6 Taarifa ya ujio wa ugeni toka nchi ya Korea Kusini

Mhe: Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inatarajia kupokea wageni kutoka nchi ya Korea Kusini hapo tarehe 31/07/2017 hadi 04/08/2017. Pamoja na mambo mengine, ugeni huu unakuja mahususi kwa ajili ya kuja kuona maendeleo ya Halmashauri katika kuendeleza kijiji cha Mfano cha Ihalalo kilichopo Kata ya Sangabuye na Iponyabugali kilichopo kata ya Kayenze**.** Aidha, wakiwa katika Halmashauri yetu, watapata fursa ya kutembelea eneo la ujenzi wa kijiji na shule mpya ya Ihalalo pamoja na kufanya kikao na Timu ya Menejimenti ya Halmashuri. Hivyo, tunawaomba viongozi na wananchi hususani walioko katika eneo litakalotembelewa kufanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya kuwapokea wageni hawa.

2.1.7 Taarifa ya ujio wa ugeni toka nchini Uingereza shule rafiki ya Ibeshi shule ya Msingi (Derby Grammer School)

Mhe: Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilitembelewa na wanafunzi 23 na viongozi 4 kutoka shule ya Derby Grammar School iliyoko London nchini Uingereza kuanzia tarehe 10/07/2017 hadi 21/07/2017. Wanafunzi hawa walikuja kufuatia uhusiano uliopo kati ya shule hiyo na shule ya Msingi Ibeshi iliyopo katika Halmashauri yetu. Pamoja na mambo mengine yaliyofanyika, ufuatao ni msaada walioutoa kwa shule ya Msingi Ibeshi:-

a. Kujenga chumba kimoja cha darasa;
b. Kutengeneza Madawati 30; na
c. Kiasi cha Tshs 5,000,000/= kilitolewa kwa ajili ya kusawazisha kiwanja cha michezo katika shule ya msingi Ibeshi iliyoko kata ya Nyakato.

Uongozi wa Halmashauri uliwashukuru viongozi na wanafunzi wa shule hiyo kwa kuichagua Ilemela kama marafiki wao wa maendeleo.

2.1.8 Taarifa ya Mikutano ya Mhe: Mbunge wa Jimbo la Ilemela.

Pamoja na shughuli nyingine Mhe: Mbunge wa Jimbo la Ilemela, alifanya Mikutano na wananchi pia aliwezesha shughuli mbalimbali za kijamii kama ifuatavyo:-

a) Usafi na Mazingira

- Kuhamasisha wananchi kulipia ada za taka; na
- Kuhimiza vijana kuunda vikundi vya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.

b) Ardhi

- Kuhimiza urasimishaji makazi holela kabla ya Master Plan kutangazwa;
- Kuhimiza utatuzi wa migogoro ya Ardhi baina ya wananchi, wananchi na Taasisi za Umma na binafsi; na

- Halmashuri ifanye uhakiki wa maeneo yote yaliyopimwa bila kuendelezwa.

c) Fedha

- Mhe: Mbunge aliagiza kutolewa kwa ilani (Notice) kwa Taasisi za Umma zinazodaiwa kodi la pango la Ardhi; na
- Mhe: Mbunge aliagiza taarifa ya kodi ya pango kuwa ya kudumu kwa kila kikao cha Kamati cha Mipango Miji.

d) Elimu Sekondari

- Ujenzi wa vyumba vya Madarasa;
- Kugawa vitabu vya Kiada na ziada; na
- Kutoa msaada wa (Computer) 20 shule ya sekondari Bugogwa.

e) Maendeleo ya Jamii

- Kuhimiza marejesho kwa vikundi vya wanawake na vijana
- Mhe: Mbunge aliwezesha mafunzo kutolewa kwa vikundi vya ujasiliamali kupitia Angeline Foundation na VETA;
- Mhe: Mbunge aliwezesha mikopo kwa vikundi vya ufugaji wa sungura; na
- Mhe: Mbunge aliwezesha upatikanaji wa mashine za kufyatulia tofali kwa kikundi cha vijana.

Naomba kuwasilisha.

John Paul Wanga,
Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa,
ILEMELA.